Je, nyota njema huonekana asubuhi?

Maoni ya wananchi kuhusu huduma za afya zinazotolewa na serikali ya awamu ya tano.

1. Utangulizi

Nchi yetu ya Tanzania inajivunia mwenendo wa matokeo mazuri ya afya. Kwa mfano, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), umri wa kuishi umeongezeka kati ya mwaka 2000 na 2012[1]. Vilevile, vifo vinavyotokana na ugonjwa wa malaria vimepungua kwa theluthi moja, wakati vifo vilivyokuwa vikitokana na maambikizi ya virusi vya ukimwi vikipungua kwa asilimia 50[2]. Mabilioni ya fedha kutoka kwa wahisani yamekuwa yakielekezwa nchini kwa lengo la kupunguza maambukizi ya ukimwi na kuboresha matibabu yake.

Hata hivyo, bado zipo changamoto nyingi katika utoaji wa huduma za afya. Mnamo Mwezi Novemba 2015[3], Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania, Dk Bill Haonga, aliwafafanulia waandishi wa habari baadhi ya changamoto wanazokumbana nazo kwenye hospitali za ngazi za wilaya, zahanati na vituo vya afya, zikiwemo upungufu mkubwa wa dawa na vifaa tiba. Hii ilikuwa baada ya ziara ya ukaguzi iliyotekelezwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. John P. Magufuli katika hospitali ya Muhimbili.

Rejea kwenye ripoti mbalimbali za utafiti kuhusiana na afya zinatoa picha ifuatayo:

- Ripoti ya Sikika mwaka ya 2013, inaonesha kuwa asilimia 94 ya hospitali zilizofanyiwa utafiti hazikuwa na aina moja ama zaidi

1 “United Republic of Tanzania: WHO Statistical Profile.” World Health Organization. WHO and UN Partners, Jan. 2015. Web.
2 ibid
3 Mtulya, Athuman. “Stakeholders Urge Magufuli to Revamp the Health Sector.” The Citizen. N.p., 12 Nov. 2015. Web.

Muhtasari huu umetayarishwa
Na kuandikwa na Twaweza Afrika Mashariki

P.O. Box 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Te: +255 22 266 4301 F: +255 22 266 4308.
uwazi@twaweza.org www.twaweza.org/sauti

Sauti za Wananchi

Twaweza ni sisi

ya vifaa muhimu vya hospitali; na asilimia 96 hazikuwa na aina moja ama zaidi ya dawa muhimu[4].

- Ripoti hii ya Sikika pia ilionesha kuwa kuna upungufu wa vitanda mahospitalini, na inaonya kwamba upungufu wa vifaa tiba, dawa na vifaa vingine utaendelea kuathiri utoaji bora wa huduma za afya nchini.
- Taasisi ya *Yale Global Health Leadership Institute* kwenye utafiti wake imegundua kuwa "kwa wastani, kitaifa, kiasi cha dawa kinachoagizwa na kupokelewa kwenye vituo vya afya vya ngazi za chini ni asilimia 60-65." Hii ina maana kuwa asilimia 35-40 ya dawa zinazoagizwa hazipatikani hospitalini[5].

Aidha, muhtasari wa *Sauti za Wananchi* wa mwaka 2013 unaonesha kuwa karibu asilimia 30 ya wahudumu wa afya hawakuwepo kazini wakati utafiti huo unafanyika na mgonjwa mmoja kati ya watatu alisubiri zaidi ya lisaa limoja kabla ya kuhudumiwa[6].

Takwimu za muhtasari huu zinatokana na utafiti wa *Sauti za Wananchi*. *Sauti za Wananchi* ni utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa (Tanzania Bara), unaotumia simu za mikononi. Taarifa zaidi kuhusu mbinu (methodolojia) za utafiti huu zinapatikana www.twaweza.org/sauti . Takwimu za muhtasari huu zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,836 kutoka kundi la pili la *Sauti za Wananchi*. Hii ikiwa ni awamu ya kumi ya kupiga simu kwenye kundi jipya. Simu zilipigwa kati ya tarehe 2 na 17 mwezi Mei mwaka 2016.

Maswali yafutayo yaliulizwa kwa njia ya simu kupitia utafiti huu wa *Sauti za Wananchi*;

1. Je, wananchi wa kawaida wanakumbana na matatizo gani wakati wanapotumia huduma za afya?
2. Je wananchi huenda wapi kupata ushauri wa kitaalamu wa kitabibu?
3. Je, wanasubiri kwa muda gani ili kumuona mtaalamu wa tiba?
4. Je, wanapata wapi dawa wanazohitaji? na
5. Je, wananchi wanaona kitu gani kuwa ndio changamoto kubwa katika sekta ya afya leo hii?

Matokeo muhimu yaliyopatikana kupitia utafiti huu zinatupa taarifa zifuatazo:

- Asilimia 61 ya wananchi huenda kwenye vituo vya afya vya serikali wanapohitaji matibabu. Hili ni ongezeko la asilimia 14 ukilinganisha na mwaka 2015.
- Asilimia 73 ya wananchi husubirishwa kwa muda wa mpaka saa moja kabla ya kumwona mtaalamu wa afya.
- Asilimia 70 ya wananchi walisema walipata baadhi ya dawa kutoka katika vituo vya afya, huku asilimia 28 wakilazimika kuzipata kwenye maduka ya dawa.

4 Report on Availability of Essential Medicines, Medical Supplies and Bed Capacity in Hospitals in Tanzania Mainland. N.p.: Sikika, n.d. Mar. 2013. Web.

5. "The Medical Stores Department. An Innovative Public Private Partnership: Medical Supply Solutions in Tanzania." Yale School of Management. Yale Global Health Leadership Institute, n.d. Web

6 Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 4, kundi la kwanza (Juni 2013)

- Asilimia 36 ya wananchi ambao wametembelea hospitali katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita wanasema zaidi ya mgonjwa mmoja hulala kwenye kitanda kimoja.
- Asilimia 59 ya wananchi wanalalamika upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya afya
- Inaonekana kuwa kuna maboresho katika sekta ya afya, ikiwemo usafi pamoja na upatikanaji wa wataalamu wa afya ukilinganisha na ripoti za wananchi ya mwezi Mei/ June 2015.
- Sera ya matibabu bure kwa wanawake wajawazito, watoto wenye umri chini ya miaka 5 (kwa ugonjwa wa malaria), na wazee haitekelezwi kikamilifu .

2. Mambo sita kuhusu huduma ya afya nchini Tanzania

Jambo 1: Wananchi 6 kati ya 10 hutembelea vituo vya afya vya serikali kupata matibabu

Asilimia 61 ya wananchi hufuata matibabu kwenye vituo vya afya vya serikali. Wengine (asilimia 16) hupata matibabu kwenye vituo binafsi ama vya mashirika yasio ya kiserikali, na asilimia 13 hununua dawa madukani. Haya ni mabadiliko chanya yanayoonesha ongezeko la watumiaji wa huduma za afya za umma. Mwaka 2015 ni asilimia 47 tu ya wananchi waliripoti kutibiwa kwenye kituo cha afya cha serikali huku asilimia 19 wakienda kwenye maduka ya dawa. Wananchi ambao hawakutibiwa kwenye vituo vya afya vya serikali walitaja sababu kuu kuwa gharama kubwa za matibabu (asilimia 43) na ugonjwa wao kutokuwa wa kuhitaji huduma ya daktari (asilimia 35)[7].

Kielelezo cha 1: Je, ni hatua gani wewe/mtu kutoka kwenye kaya yako alichukua ili kutibu ugonjwa ama jeraha?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)
Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 32 (Mei/Juni 2015).
Baadhi ya takwimu za mwaka 2015 hazijaoneshwa

7 Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)

Jambo 2: Wananchi 7 kati ya 10 husubiri zaidi ya lisaa limoja kumuona mtaalamu wa afya

Wananchi wengi (asilimia 73) waliotembelea vituo vya afya (binafsi, serikali ama cha mashirika yasiyo ya kiserikali) walisubiri kwa muda usiozidi lisaa limoja kabla ya kumuona mtaalamu. Wengi wao walikiri kuwa mtaalamu wa afya aliwaelezea kwa kina kuhusu ugonjwa wao (asilimia 90) na baada ya hapo, aliwaandikia dawa (asilimia 81)[8].

Kielelezo 2: Je, wewe/mtu kutoka kwenye kaya yako alisubiri kwa muda gani kabla ya kupata huduma?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)

Jambo la 3: Wananchi 7 kati ya 10 hupata dawa kutoka kwenye kituo cha afya

Wananchi 7 kati ya 10 (asilimia 70) walisema kwamba walipata baadhi ya dawa kwenye kituo cha afya, lakini wananchi 3 kati ya 10 (asilimia 28) walilazimika kwenda kununua dawa kwenye duka la dawa.

Kielelezo cha 3: Je wewe/mtu kutoka kwenye kaya yako alipata wapi dawa alizoandikiwa?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)

8 ibid

Jambo la 4: Wananchi 4 kati ya 10 walioenda hospitali katika miezi kumi na mbili iliyopita waliripoti kushuhudia mgonjwa zaidi ya mmoja akitumia kitanda kimoja

Mwaka jana asilimia 46 ya wananchi walilazwa au walimsindikiza mtu aliyelazwa hospitali[9]. Watatu kati ya kumi walisema hakukuwa na vitanda vya kutosha (asilimia 31), mashuka ya kutosha (asilimia 27), na vyandarua vya kutosha (asilimia 29) katika wodi walizolazwa[10]. Vilevile, asilimia 36 ya wananchi walikiri kushuhudia mgonjwa zaidi ya mmoja akitumia kitanda kimoja. Mwaka 2015 walioshuhudia tatizo hili walikuwa ni asilimia 30. Kwa wale walioshuhudia mgonjwa zaidi ya mmoja akitumia kitanda kimoja mwaka huu (2016), asilimia 13 walisema ilizoeleka kuona kitanda kimoja kikitumiwa na wangonjwa watatu.

Kielelezo cha 4: Je mgonjwa anatumia kitanda ama godoro na mgonjwa/wagonjwa wengine?



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 10 (Agosti 2016)

Jambo la 5: Watu 6 kati ya 10 wanasema ukosefu wa dawa au vifaa tiba vingine kwenye vituo vya afya vya serikali ni changamoto kubwa

Asilimia 58 ya wagonjwa walitibiwa katika vituo vya afya vya serikali ndani ya miezi mitatu iliyopita[11]. Walipoulizwa kuhusu matatizo waliyokutana nayo, asilimia 59 walitaja tatizo la ukosefu wa dawa/vifaa tiba. Hakuna mabadiliko makubwa katika hali hii tangu mwaka 2015.

Idadi ya waliolalamikia kutokuheshimiwa na wahudumu ilishuka kutoka asilimia 42 (2015) mpaka asilimia 27 (2016). Vilevile, ni asilimia 11 tu waliolalamikia kuwa vituo vya afya ni vichafu, ukilinganisha na asilimia 29 mwaka 2015. Waliotaja ukosefu wa madaktari kama changamoto walipungua kutoka asilimia 43 (2015) mpaka asilimia 18 (2016).

9 ibid
10 ibid
11 Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu 10 (Julai 2016)

Kielelezo cha 5: Je ulipata tatizo lolote kati ya haya wakati ulipoenda kwenye kituo cha afya



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)
Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 32 (Mei/Juni 2015).

Jambo la 6: Wananchi 4 kati ya 10 wanafahamu wazee (60+) ambao wamelipia matibabu kwenye vituo vya afya vya serikali

Ingawa Sera ya Afya ya Tanzania inaorodhesha kwa msisitizo kabisa, makundi ambayo hayapaswi kulipia matibabu kwenye vituo vya afya vya serikali, bado sera hii haitekelezwi kikamilifu. Makundi haya yanahusisha matibabu ya ugonjwa kwa wazee (wenye umri wa miaka 60+), wajawazito, na watoto chini ya miaka mitano (5). Hata hivyo, wananchi walipoulizwa iwapo wana taarifa juu ya matibabu ya bure kwa makundi haya, majibu yao yalikuwa yafuatayo: Wananchi wanne kati ya kumi walisema wanafahamu wazee ambao walilipia matibabu kwenye vituo vya afya vya serikali. Vilevile, asilimia 35 walisema wanafahamu kisa cha mtoto wa chini ya miaka mitano aliyelipia dawa za malaria na asilimia 28 ya wananchi waliwajua wanawake wajawazito ambao walilipia matibabu yao.

Kielelezo cha 6: Makundi yasiyopaswa kulipia matibabu (wengi wao bado wanalipia)



Chanzo cha Takwimu: Utafiti wa *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 10 (Agosti 2016)

3. Hitimisho

Muhtasari huu unajumuisha maoni ya wananchi juu ya sekta ya afya nchini Tanzania. Inaonekana kuwa kumekuwa na maboresho kadhaa kwenye sekta ya afya kwani wananchi wanasema wapo wahudumu wazuri, wenye maadili na walio makini tangu mwaka 2015.

Hata hivyo, malalamiko bado yanasikika. Zahanati, hospitali za wilaya, na vituo vya afya vinatajwa kama vituo visivyokuwa na ubora, vifaa tiba vya kutosha na vyenye upungufu wa dawa. Mifumo ya manunuzi na usambazaji wa vifaa tiba na dawa haifanyi kazi ipasavyo; pesa zinazotolewa hazitoshi; na hakuna uwajibikaji baina ya watumishi wanaofanya manunuzi hayo. Ili kushughulikia suala hili, inapaswa kupitia kwa umakini sera mbalimbali na kuelewa vikwazo vilivyopo. Vilevile, kutahitajika kupanga kwa makini mikakati itakayosaidia kuvishughulikia.

Muhtasari unaohusu sababu za uhaba wa madawa wa Taasisi ya Maendeleo ya Nje (*Overseas Development Institute - ODI)* na Twaweza umeainisha changamoto kadhaa kwenye sekta ya afya[13] hususani:-

- Kutilia mkazo kwenye mabadiliko yanayoonekana kwa mfano kujenga vituo vya afya badala ya kujikita tu kwenye kuagiza na kupeleka dawa.
- Wahudumu wengi kujikita kwenye maeneo ya mijini na kukosekana kwa ujuzi wa kutosha miongoni mwa wahudumu.
- Upungufu wa wahudumu katika maeneo yasiyo ya mijini.
- Wananchi na mamlaka kutokuwa na taarifa za uhakika kuhusu dawa zilizopo na zinazohitajika. Kugundua uhitaji wa dawa kwa wakati, ufahamu wa viwango vinavyohitajika na mbinu bora za manunuzi, yote ni masuala muhimu.

12 Japokuwa sera inasema kwamba matibabu yote kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano ni ya bure, wahojiwa waliulizwa kuhusu matitbabu ya malaria tu.

13 What role can citizens play in reducing stock outs, Twaweza, May 2014 http://www.twaweza.org/uploads/files/CitizensStockOuts-ODI+Twaweza-EN-FINAL.pdff

- Ukosefu wa rasilimali.
- Kukosekana kwa utamaduni wa uwajibikaji; vitendo vya rushwa kutokuripotiwa na kutokuchunguzwa , mifumo ya usimamizi wa utendaji ni duni na hakuna motisha kwa watoa huduma.

Katika kipindi kijacho, masuala haya yatahitajika kufanyiwa kazi. Suala la bajeti lazima litahusika, hususani katika kupambana na upungufu wa vifaa vya kutolea huduma ya afya kama vile dawa. Utafiti wa Twaweza wa majaribio kwenye elimu, KiuFunza, umeonyesha matokeo yanayofanana ya kuwa; ongezeko la rasilimali shuleni linapokwenda sambamba na utoaji wa motisha kwa walimu (bakshishi ya fedha), huchangia matokeo ya ujifunzaji kuwa mazuri. Hata hivyo, maboresho yaliyoanishwa katika utoaji wa huduma za afya na takwimu hizi za *Sauti za Wananchi* ni hatua za kupongezwa katika kuelekea kwenye Tanzania yenye huduma bora za afya.